

## Maelezo ya Ukweli Kuhusu COVID-19 Usalama na udhabiti wa kinga ya chanjo za COVID-19

Ugonjwa wa COVID-19 unaweza kuwa [na athari sugu na zenye kuhatarisha maisha](#), na hakuna namna ya kufahamu vipi virusi vya COVID-19 vitaathiri kila mtu. Chanjo zote tatu [za COVID-19](#) zinazopatikana nchini Marekani zimethibitishwa kuwa salama na dhabiti katika **kuzuia maradhi makali, kulazwa hospitalini, na mauti yanayotokana na ugonjwa wa COVID-19**.

Hatua ya kwanza katika kufanya maamuzi ya iwapo utapata chanjo ni kupata [habari sahihi na za kuaminika](#). Habari zinazofuata zimetoka kwa wataalamu tajika kutoka kwa [Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa \(CDC\)](#), mamlaka [ya Usimamizi wa Chakula na Dawa \(FDA\)](#), Taasisi [ya Kitaifa ya Sayansi, Uhandisi na Matibabu \(NASEM\)](#), Shirika [la Afya Duniani \(WHO\)](#), na [Idara ya Afya na Huduma za Binadamu \(HHS\) ya Marekani](#).

### ***Chanjo za COVID-19 zina uwezo wa kiasi gani wa kuzuia virusi hivi?***

Chanjo za COVID-19 kutoka kwa makampuni ya [Pfizer-BioNTech](#), [Moderna](#) na [Johnson & Johnson \(Janssen\)](#) zimeidhinishwa kwa matumizi ya dharura na mamlaka ya FDA, huku shirika la CDC likipendekeza matumizi yazo. Wakati wa tafiti, ilibainika kwamba chanjo hizo **zilizuia madhara makali ya ugonjwa wa COVID-19** kwa ufanisi wa viwango vya juu. Wataalamu wakuu wa kitaifa wanasema kwamba kuna changamoto katika kulinganisha viwango vya ufanisi wa chanjo kutoka kwa tafiti za kliniki kati ya chanjo hizo tatu kwa sababu kila moja ya chanjo hizo haikufanyiwa majaribio ikilinganishwa na nyingine, wala majaribio hayakufanyika katika hali au nyakati sawa. Shirika la CDC linapendekeza kwamba upewe chanjo ya kwanza unayoweza kupata ili upate kinga dhidi ya COVID-19.

### ***Ninaweza kuambukizwa COVID-19 kupitia chanjo?***

Hakuna chanjo yoyote ya COVID-19 kati yazo inayoweza kusababisha maambukizi ya COVID-19. Chanjo hutayarisha kinga asili za mwili ili kupambana na virusi mahususi. [Chanjo za COVID-19 hutumia mbinu tofauti](#) ili kutimiza lengo sawa, ambalo ni kutumia **sehemu** ya kirusi isiyo na madhara ambayo husababisha COVID-19 – protini ya utando hujigandisha kwenye seli – ili kuufundisha mwili jinsi ya kutambua protini hiyo, na kujikinga dhidi yayo ikiwa itakabiliana nayo tena baadaye.

[Chanjo za Messenger RNA \(mRNA\)](#), zikijumuisha ile ya Pfizer na Moderna hazitumii virusi hai. Zinafunza seli jinsi ya kuunda protini ambayo huchochea kuwezesha kwa kinga katika mwili. [Chanjo zinazowasilisha chembejeni katika seli](#), ikiwemo chanjo ya Janssen, hutumia virusi vilivyobadilishwa visivyo na madhara (kama vile vya mafua) ili kuwasilisha maagizo kwenye seli. Chanjo hiyo haiwezi kusababisha maambukizi ya COVID-19 au kwa kutumia kirusi kisicho hai kinachotumika kama kisafirishaji.

### ***Chanjo hizi za COVID-19 ni salama kwa kiasi gani?***

Katika mchakato mzima wa kubuniwa na kuidhinishwa kwa chanjo, [usalama umepewa kipaumbele](#). Usalama wa chanjo unaendelea kupewa kipaumbele huku chanjo zikiendelea kutolewa, kupitia mikakati endelevu ya kuchunguza viwango vya usalama.

- **Majaribio ya viwango vya juu:** Mchakato [wa utengenezaji wa chanjo ya COVID-19](#) ulijumuisha hatua zinazolingana na zile zinazotumiwa kutengeneza chanjo za awali, kama vile chanjo ya homa na surua. [Majaribio ya chanjo kwa watu hutumika kutafiti kuhusu usalama na ufaafu wa chanjo miongoni mwa maelfu ya washiriki wa tafiti](#). Hakuna masuala makuu ya kutilia shaka usalama wa chanjo hizo yaliibuka wakati wa majaribio hayo.
- **Tathmini za hali ya juu:** Mamlaka ya FDA hutumia viwango vya juu na ushauri kutoka kwa wataalamu huru wa matibabu ili kutathmini data zote zilizopo na kuhakikisha kwamba chanjo ni [salama na faafu, na kwamba manufaa ya matumizi yake yanazidi hatari zozote zinazoweza kutokana na kutumia chanjo hiyo](#). Baada ya FDA kutoa maamuzi, shirika la CDC pia hupitia data zilizopo kabla ya kutoa mapendekezo ya mwisho kuhusu matumizi ya chanjo.
- **Uchunguzi endelevu wa usalama wa chanjo:** Shirika la CDC pamoja na wabia wengine wa shirikisho wanaendelea kuchunguza chanjo mpya ili kubaini ikiwa zina athari zozote kali, kwa kutumia mifumo mbalimbali ya kuchunguza usalama wa chanjo. Uchunguzi huu endelevu unaweza kufichua athari ambazo huenda hazingekonekana wakati wa majaribio.

Katika majaribio matatu ya chanjo, kulikuwa na zaidi ya washiriki 116,000. Wakati Dkt. Jerome Adams alipokuwa anahudumu kama mkuu wa afya ya umma nchini Marekani, alisema kwamba tafiti za kawaida huwa na takriban washiriki 5,000 baada ya chanjo kuidhinishwa, huku akieleza kwamba, "Wakati chanjo hizi zitakuwa zikitolewa kwa wakazi wa Marekani, zitakuwa na data nyingi kuliko chanjo nyingine yoyote katika historia."

### **Chanjo za COVID-19 ziliwezaje kubuniwa haraka hivyo?**

Hapo awali, ilichukua miaka mingi kubuni chanjo. Mchakato wa kubuni chanjo za COVID-19 umekuwa wa haraka kwa sababu mbalimbali. Hakuna hatua zilizoachwa, lakini watafiti waliendesha hatua zingine za mchakato huo kwa wakati mmoja. Hatua hizi zilijumuisha awamu za majaribio zilizoendeshwa kwa wakati mmoja na nyakati za majaribio zilizofupishwa ili kupunguza muda wa kusubiri. Kwa kuwa COVID-19 hutokana na jamii ya virusi, ikijumuisha virusi vya SARS vya mwaka wa 2002 na virusi vya MERS vya 2012, wanasayansi tayari walikuwa wamefanya utafiti kuhusu sifa za virusi mbalimbali vya coronavirus na kuanza kutengeneza chanjo sawa. Jambo hili liliwezesha kubuniwa kwa haraka kwa chanjo za COVID-19.

### **Chanjo za COVID-19 ni salama kwa makundi yote ya watu?**

Majaribio ya kimatibabu ambayo yalitafiti ufanisi na usalama wa chanjo ni pamoja na watu wa asili mbalimbali, ikiwa ni pamoja na jamii ambazo kihistoria zimewakilishwa kwa kiwango cha chini katika utafiti wa kimatibabu. Jamii hizi pia zimeathirika na COVID-19 katika namba zisizo sawa. Takriban [asilimia 42 ya washiriki wa majaribio ya Pfizer BioNTech yaliyofanyika kote ulimwenguni](#), [asilimia 37 ya washiriki wa Moderna](#), na [asilimia 35 ya washiriki wa Johnson & Johnson \(Janssen\)](#) walikuwa watu kutoka jamii zisizo za wazungu, ambazo huashiria uanuwai wa kijamii nchini Marekani.

Kando na hilo, tafiti za kimatibabu zilihusisha watu wazee walio hatarini zaidi [asilimia 21 ya washiriki wa Pfizer-BioNTech, asilimia 23 ya washiriki wa Moderna, asilimia 34 ya washiriki wa Johnson & Johnson (Janssen)]; na watu wenye magonjwa sugu yanayowaweka katika hatari kubwa iwapo wataambukizwa COVID-19 [asilimia 46 ya washiriki wa Pfizer-BioNTech, asilimia 42 ya washiriki wa Moderna, na asilimia 40 ya washiriki wa Johnson & Johnson (Janssen) participants].

Watoto pamoja na wanawake wajawazito au wanaonyonyesha hawakuhushwa kwenye majaribio ya kliniki, hivyo hakuna data zinazopatikana kwa wakati huu kuhusu usalama wa chanjo hizi kwa makundi hayo ya watu. Majaribio ya chanjo kwa makundi haya yanaendelea au yanaanza hivi karibuni.

### **Manufaa ya kupata chanjo ya COVID-19 ni yapi?**

Chanjo za COVID-19 huwapa watu kinga bila kuwaingiza katika hatari ya kupata magonjwa. Watu ambao waliambukizwa COVID-19 hapo awali huenda wakapata kinga ya muda mfupi kutoka kwa kingamwili, lakini haijulikani kinga hiyo itadumu kwa muda gani. Dalili za ugonjwa wa COVID-19 huenda zikawa tofauti sana, kuanzia dalili za kiwango kidogo hadi dalili sugu, na huenda zikadumu kwa muda mrefu na zenye kuhatarisha maisha. Kupokea chanjo kutakulinda kwa kubuni mfumo wa kinga utakaokabili virusi hivyo bila kukufanya mgonjwa.

Chanjo za COVID-19 zinaweza kuzuia usidhurike sana iwapo utaambukizwa virusi hivi. Ni muhimu sana kujikinga dhidi ya COVID-19 kwa kuwa kwa watu wengine, virusi hivi vinaweza kusababisha maradhi makali au kifo..

### **Kupokea chanjo za COVID-19 kuna athari gani?**

Athari zinazoshuhudiwa zaidi [baada ya kupokea chanjo za COVID-19](#) ni sawa na athari zinazoonekana baada ya kupokea chanjo nyingi. Utakapopokea chanjo ya COVID-19, huenda ukashuhudia athari ndogo kama vile: maumivu, wekundu, au kufura kwenye eneo lililodungwa; homa na/au kuhisi baridi; kuumwa na kichwa; uchovu; na maumivu ya misuli na maungo. Ni kawaida kushuhudia athari hizi na ni ishara kwamba mwili wako unapata kinga ya kukulinda dhidi ya COVID-19. Kwa kawaida athari hizi hushuhudiwa kwa siku chache tu, na huenda zikaongezeka baada ya kupokea dozi ya pili.

### **Kumekuwa na wasiwasi wowote kuhusu usalama wa chanjo za COVID-19?**

[Athari kali za mizio](#), kama vile mmenyuko wa mizio ambapo mtu anahitaji kutibiwa kwa epinephrine au kulazwa hospitalini, ni nadra. [Uwezekano wa kupata athari mbaya za chanjo huongezeka ikiwa una hali fulani za kiafya](#), kama vile mfumo dhaifu wa kinga, au ikiwa umeshuhudia mizio baada ya kupata chanjo nyingine hapo awali. Shirika la CDC linafahamu kuhusu idadi ndogo ya watu ambao wameshuhudia [athari kali](#) baada ya kupata chanjo ya COVID-19 ya mRNA.

### **Kuna mtu yeyote ASIYEFAA kupata chanjo ya COVID-19?**

Ndiyo, kuna hali chache ambapo kutolewa kwa chanjo hizi hakupendekezwi.

- **Watu wanaopata mizio mikali baada ya kupata chanjo:** Watu wenye historia inayofahamika ya [kushuhudia mizio mikali](#) inayosababishwa na viungo vyovyote vya chanjo au mtu yeyote aliyepata mizio mkali baada ya kupokea dozi ya kwanza ya COVID-19 **HAFAI** kupata chanjo.
- **Watu wenye mizio wa PEG au polysorbate:** Polysorbate sio kiungo katika chanjo yoyote ya mRNA ya COVID-19 vaccine lakini inahusiana kwa karibu na PEG, ambayo imo kwenye chanjo zote mbili za mRNA. Watu wenye [mizio wa PEG au polysorbate](#) hawafai kupata chanjo ya mRNA.
- **Watu ambao sasa hivi wanagua COVID-19 au wako katika karantini:** Ikiwa sasa hivi unagua COVID-19, subiri hadi utakapopona na kutimiza vigezo vya CDC [vitakavyokuruhusu kuacha kujitenga nyumbani](#). Ikiwa huenda umeambukizwa COVID-19 na uko katika karantini, subiri hadi kipindi chako cha kukaa katika karantini kitakwisha ili usihatarishe kuwaambukiza wengine.

*Ilisishwa mnamo Machi 4, 2021.*

Kwa maelezo ya ziada, tembelea [coronavirus.ohio.gov](https://coronavirus.ohio.gov) au upige simu kupitia 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634).